

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA
SHULE YA SEKONDARI KISHISHA S.L.P 171
SANYA JUU- SIHA

Kumb Na. KSS/ ADM/REG/20.....

Jina la
mwanafunzi.....
..

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KISHISHA
WILAYA YA SIHA, MKOA WA KILIMANJARO MWAKA

1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha..... katika shule ya sekondari kishisha mwaka 20.....
Shule ipo umbali wa km karibu na shule ya msingi kishisha
Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe/...../20.....
Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe...../...../20.....
saa.....

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

a) Sare za shule

- (a) Wavulana suruali mbili(02) za kitambaa cha rangi ya UDONGO zenye rinda mbili mbele, upana wa chini usiwe pungufu ya inchi 16
- (b) Wasichana watashona sketi mbili za rinda box ambazo zitatakiwa kuvuka chini ya magoti kiasi cha urefu wa **inchi 10** na sweta ya rangi ya UDONGO
- (c) Shati nyeupe ya mikono mifupi mbili ,soksi nyeupe kwa wasichana jozi 03 na soksi nyeusi kwa wavulana jozi 03 na viatu vyeusi vya ngozi visivyo na visigino virefu, pia ni lazima view vya kufunga kwa kamba
- (d) Wale wanaovaa hijabu wavae sketi ndefu, shati na hijabu nyeupe.

b) Mahitaji ya darasani

madaftari counter books 2 quire 03, daftari ndogo 09 kwa ajili ya majaribio ya kila wiki, mkebe wa hesabu, kalamu za kutosha, pencil, rula na vifutio.

c) Huduma ya chakula

shule kwa kushirikiana na wazazi wameweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha wanafunzi wanapata chakula cha mchana shuleni

3.0 Sheria na kanuni muhimu ya shule hii

- shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatiwa miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya Rais –TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.
- Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripori shuleni:
 - i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo lazima.
 - ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
 - iii. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni(preparation)
 - iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule na utakazopewa
 - v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingayia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
 - vi. Kutunza usafi wamwili, mavazi na mazingira ya shule.
 - vii. Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa
 - viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
 - ix. Kutunza mali za umma

3.2 Makosa yafuatayo yaweza kusababisha kufukuzwa shule au kusimamishwa shule:

- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika
- e) Kupigan au kupiga
- f) Kuharibu kwa makusudi mali za umma
- g) Kudharau Bendera ya Taifa
- h) Kuwa mjamzito au kusababisha mimba
- i) Kuo au kuolewa
- j) Kutoa mimba
- k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi

m) Kuwa na simu


n) Utoro na kujificha vichakani wakati wa masomo


4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi

- a) Fomu ya uchunguzi wa kiafya [medical examination form] ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutokushiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo /maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

NB: -Kwa mzazi yeyote ambaye atampeleka mtoto wake shule ya binafsi anatakiwa alete uthibitisho kamili wa usajili wa mwanae toka shule husika


KARIBU SANA
ELISANTE M. MBARI
.....
MKUU WA SHULE


MKUU WA SHULE YA SEKONDARI
KISISIYA